Maoni



# HSNP2:
## Mwongozo wa Nyanjani

**Kufungua akaunti ya benki, kupokea kadi za ATM, Uandikishaji wa vitambulisho vya taifa na Kusuluhisha matukio maaluum**



# Madhumuni


Mwongozo wa nyanjani wa kutumiwa na timu za Kaunti za HSNP2.......................................................3

I. Wajibu na Majukumu.......................................................3
II. Matayarisho ya ufunguzi wa akaunti ya Benki.......................................................3
III. Hatua ya ufunguzi wa akaunti ya Benki.......................................................3
Hatua ya 1: RC, Mtu wa Kujitolea na Msimamizi wa Benki ya Equity kukutana Na Chifu au Msaidizi wa Chifu (Siku ya kwanza ya Kazi ya Nyanjani).......................4
Hatua ya 2: RC, Mtu wa Kujitolea na timu ya Benki ya Equity Kuandaa eneo la kufanyia kazi.......................................................4
Hatua ya 3: Chifu au Msaidizi wa Chifu afungue mkutano wa kutoa Ujumbe kwa jamii.......................................................5
Hatua ya 4: RC au mtu wa kujitolea anatoa Ujumbe wa Mradi wa HSNP2 .................................5
Hatua ya 5: Msimamizi wa Benki ya Equity ashiriki Ujumbe Muhimu wa Benki.........................6
Hatua ya 6: Ukusanyaji wa data na utoaji wa Kadi.......................................................7
Hatua ya 7: Msimamizi wa Benki ya Equity afunge eneo la kazi ya nyanjani...............................7
Hatua ya 8: Msimamizi wa Benki ya Equity na RC waripoti matatizo Au masuala yoyote.......................................................7

Ujumbe muhimu wa Ufunguzi wa akaunti ya Benki...............................................8
Kuna aina nne (4) za kutoa ujumbe muhimu wakati wa mkutano wa Jamii:........................................8
I. Ujumbe muhimu wa mradi wa HSNP: unatolewa na Chifu au Msaidizi wa Chifu.............................8
II. Ujumbe wa kindani wa mradi wa HSNP: unatolewa na RC au mtu wa kujitolea...............................9
III. Ujumbe wa Benki: Utatolewa na Msimamizi wa Timu ya Nyanjani wa Benki ya Equity....................11
IV. Ujumbe kuhusu haki yako.......................................................10

Mwongozo wa kutatua matukio maalum wakati wa ufunguzi wa akaunti ya Benki
.......................................................8






b) Waelezee kuwa nambari sahihi ya Kitambulisho cha Taifa lazima iandikwe na Kuthibitishwa tena na Benki kabla ya akaunti ya Benki kufunguliwa;

c) Jaza Fomu ya kisahihisha pamoja na Mwakilishi, na kuandika nambari sahihi ya Kitambulisho cha Taifa.
Hili suala lazima lijulishwe kwa Afisa Msimamizi wa Msaada wa Data (DMO) haraka iwezekanavyo (au moja kwa moja kwa Mratibu wa Kaunti ndogo (Zonal Manager ikiwa yupo).

## 5 Mtu ana maswali kuhusu wale ambao watapata malipo ya dharura, wakati wa ukame au dharura kama hiyo.

a) Mwelezee Mtu binafsi kuwa kiasi cha pesa kinachopatikana kwa malipo ni kidogo, kwa hivyo walio na shida zaidi ndio watakaopewa kipaumbele kupokea malipo yoyote ya ziada ya dharura;

B) Waeleze kuwa ikiwa malipo ya dharura yatafanywa, yatatangazwa mapema. Wale ambao watapata malipo na vile kiasi cha malipo kitakuwa, itategemea sababu nyingi, Ikiwa ni pamoja na makali ya ukame au suala hilo la dharura.



## 3. Mwakilishi hayuko kwenye Orodha ya Benki ya Equity.
*Kuna uwezekano wa mambo mawili (2):*

***i. Nyumba ilikosa kuandikishwa wakati wa usajili na haiko katika data ya Benki ya Equity (aidha kama Mwenye Kitambulisho au Asiye na Kitambulisho);***

a) Elezea jamaa wote wa nyumba kuwa hatua zote zilifanywa kuwapata watu wote wakati wa usajili, lakini baadhi ya nyumba zilikosa kusajiliwa kutokana na idadi kubwa wa eneo hilo, nyumba zingine zilikuwa zimehama wakati wa kiangazi;

b) Waeleze kuwa ni sharti mtu mmoja wa nyumba yao awe na kitambulisho halali cha Taifa..

***ii. Mtu huyu si mmoja wa Mwakilishi andikishwa wakati wa Usajili, ni lazima idhibitishwe na Nyumba kuwa ni Mwakilishi halali;***

a) Mwelezee kuwa Mwakilishi anayefungua akaunti ya Benki anapaswa kuwa mmoja wa jamaa wa nyumba aliyetambuliwa wakati wa usajili.

b) Mwelezee kuwa lazima amueleze aliye sajiliwa kama Mwakilishi ahudhurie kufunguliwa kwa Akaunti ambapo shughuli hiyo inaendelea katika sub-lokeshi lao. Ikiwa haiwezekani, mwakilishi anaweza pia kufungua akauti katika eneo lolote shughuli hiyo inaendelea ama ikiwezekana, akafungue akaunti katika tawi la benki la Equity la Kaunti lao.

c) Waeleze kuwa ikiwa familia ingetaka kubadili Mwakilishi, ombi linaweza kutumwa kwa RC ambao watawakilisha ombi lao kwa fomu la "update", lakini wanaweza kuchelewa kufungua akaunti ya benki, kwani kazi ya kufanya hivyo unahusisha hatua nyingi.

## 4. Nambari ya Kitambulisho cha Taifa cha Mwakilishi Iliandikishwa kimakosa wakati wa usajili (*Mwakilishi anaamini yeye alitoa Kitambulisho cha halali cha Taifa Wakati wa Usajili*).

a) Mwelezee Mwakilishi kuwa ataweza kufungua akaunti ya Benki akitumia Risiti ya usajili wa Nyumba zinazotolewa, na kuwa akaunti hii inaweza kuwezeshwa kwa muda wa wiki tatu (3) baada ya kuwasilisha Kitambulisho cha Taifa kwa agenti.



# Mwongozo wa nyanjani wa kutumiwa na timu za Kaunti za HSNP2

Tofauti na mkondo wa kwanza wa ufunguzi wa akaunti za HSNP2, kwa mkondo wa pili, mtindo utakuwa wa haraka ambapo kadi za ATM zitatolewa papo hapo. Mwongozo huu unatoa maelezo ya msingi kwa timu za HSNP2 Kaunti kuhusu jinsi ya kutekeleza ufunguzi wa akaunti ya Benki na Utoaji wa Kadi wakiwa kwa jamii.

**Timu ya Kauti ya HSNP2 ya ufunguzi wa akaunti ya Benki na utoaji wa Kadi ina:**

- ☐ Chifu au Msaidizi wa Chifu
- ☐ Mtu wa Kujitolea wa HelpAge
- ☐ Mwanachama wa kamati ya haki ya HelpAge (RC)
- ☐ Timu ya Benki ya Equity: Watu 3 wakiongozwa na msimamizi

## I. Wajibu na Majukumu
Kila mwanachama wa timu ya HSNP2 Kaunti ana majukumu ya kipekee ya kutimiza wakati wa ufunguzi wa akaunti ya Benki na utoaji wa Kadi:

## II. Matayarisho ya ufunguzi wa akaunti ya Benki
Kabla ya kufungua akaunti ya benki na kupewa kadi, mhudumu wa kujitolea na Mwanakamati wa HelpAge (RC), Chifu, Naibu wa Chifu na Wasimamizi wa Benki, lazima wahakikishe kuwa wana vifaa vyote vinavyohitajika:

**RC na Mhudumu wa Kujitolea**

- Orodha Wakilishi wa Nyumba ya HSNP
- Maelezo ya HSNP
- Fomu ya Malalamishi
- Fomu za mambo mapya
- Bahasha Kubwa
- Penseli/kalamu ya wino
- Dawati + Kiti, ikiwa zahitajika

**Msimamizi wa Benki ya Equity**

- Ordha ya Wateja
- Fomu za Kufungua akaunti ya Benki
- Kompyuta
- Mashine za kupiga nakala (Hati + Alama za Vidole)
- Kamera Dijitali
- Kamba za kugawanya/vijiti
- Madawati + Viti, ikiwa yahitajika
- Mashine na Programu za Kuunda Kadi

Ikiwezekana, mwanakamati wa RC, mhuduma wa kujitolea na timu ya Benki ya Equity, lazima washirikiane kugawana uchukuzi (transportation) ili kuhakikisha kuwa kikosi cha watu wote kinawasili kwa wakati unaofaa.

## I. Hatua ya ufunguzi wa akaunti ya Benki

### **Hatua ya 1:** RC, Mtu wa Kujitolea na Msimamizi wa Benki ya Equity kukutana na Chifu au Msaidizi wa Chifu (Siku ya kwanza ya Kazi ya Nyanjani)

Mara wanapofika nyanjani, timu itakutana ili kupanga jinsi ya kufanya kazi. Pia, watamjulisha Chifu au Msaidizi wa Chifu mpangilio wa kazi na *Ujumbe Muhimu wa Msingi*.

### **Hatua ya 2:** RC, Mtu wa Kujitolea na timu ya Benki ya Equity kuandaa eneo la kufanyia kazi

a) RC anaandaa pahali pa kupokea msaada (Help Desk) katika eneo tofauti na pahali timu ya Benki ya Equity itapakokuwa ikifungua akaunti. Hata hivyo, lazima pawe mahali rahisi kutambuliwa kwa urahisi na wanaohudhuria.

b) Kikosi cha benki kitenge sehemu ya makaribisho na zile sehemu tatu za Benki ya Equity kwa mlolongo (assembly line). Msimamizi wa Benki ya Equity na mwanakamati wa RC wahakikishe kuwa kila pahali pa msaada na pahali pa watu kutunga mlolongo pana nafasi ya kutosha.





## Mwongozo wa kutatua matukio maalum wakati wa ufunguzi wa akaunti ya Benki

Mwongozo huu unanuiwa kuwasaidia RC na watu waliojitolea (volunteers) kukabiliana na matukio maalum na masuala yasiyotarajiwa wakati wa kazi ya ufunguzi wa akaunti ya Benki.

Ni muhimu kwa watu waliojitolea na RC waripoti masuala yoyote yanayotokea ambayo hayajaelezewa katika mwongozo huu kwa mratibu (system) wao wa SPR ili mwongozo huu uboreshwe.

### 1 Mwakilishi alisahau Kadi ya Kitambulisho cha Taifa na Risiti ya usajili wa Nyumba na hawezi kufungua akaunti leo.

a) Elezea kuwa Benki ya Equity kisheria inahitajika kukagua Kadi ya Kitambulisho cha Taifa au Risiti ya wsajili wa Nyumba wa kila Mwakilishi.

b) Mshauri Mwakilishi kurudi na Kitambulisho chake cha Taifa au Risiti ya usajili wa Nyumba wakati kazi ya nyanjani inapoendelea katika lokisheni ndogo yake au iliyo karibu wakati wa kazi ya nyanjani inayofuata.

### 2. Kadi ya Kitambulisho cha Taifa cha Mwakilishi imepotea, Imeharibika au imeibiwa.

a) Mwelezee Mwakilishi kuwa HSNP haina uwezo wowote kwa utoaji wa Vitambulisho vya Taifa. Halmashauri ya Usajili la Taifa (NRB) ndiyo ina wajibu huu, na ina sheria zake.

b) Mshauri Mwakilishi kwenda kwa NRB kuchukua tena Kitambulisho cha Taifa wakati wa shughuli ya usajili wa Vitambulisho.

c) Waeleze kuwa itawabidi kusubiri hadi Kadi zao za Kitambulisho cha Taifa Zitakapotolewa.


d) RC au mtu wa kujitolea ataweka orodha ya nyumba zenye masuala ya aina hii.

- Baada ya akaunti yako kuwezeshwa, na pesa kuwekwa, si lazima la kutoa pesa zote. Pesa zitawekwa salama katika akaunti yako na unaweza kuzipata wakati wowote ila tu uwe umetumia akaunti yako katika mwiezi sita (6).

- Mpango huo utatoa malipo mara mbili katika kipindi kimoja. Hata hivyo, zaidi ya hayo, utatozwa malipo ya kawaida ya shughuli za benki.

- Kama unahitaji kutumia akaunti yako kwa ajili ya shughuli nyingine zaidi isipokuwa shughuli za HSNP utatozwa malipo ya kawaida za benki.

- Kama una malalamiko kuhusu upataji wa pesa zako, tafadhali toa ripoti kwa RC wako au agenti wa malipo ya Equity. Unaweza pia kupiga simu kwa nambari iliyo nyuma ya kadi yako ya malipo. Kupiga simu kwa nambari hiyo hakulipishwi. Kumbuka kutambua nambari ya kumbukumbu (reference number) itakayotolewa unapopiga simu, itatuwezesha kufuatilia suala lako kwa makini.





## **Hatua ya 3:** Chifu au Msaidizi wa Chifu afungue mkutano wa kutoa Ujumbe kwa jamii

a) anafungua mkutano wa kutoa ujumbe kwa jamii kama kawaida;

b) anaitambulisha timu ya nyanjani na;

c) anashiriki *Ujumbe Muhimu wa Mradi wa HSNP.*
Ni muhimu ikiwezekana mkutano huu uwe mfupi ili kuhakikisha kuwa wote Waliohudhuria wanahudumiwa katika muda uliopangwa.

## **Hatua ya 4:** RC au mtu wa kujitolea anatoa ***Ujumbe wa Mradi wa HSNP2*** *kwa* wanaohudhuria mkutano wa jamii

a) RC au mtu wa kujitolea atoa *Ujumbe wa Mradi wa HSNP* kwa waliohudhuria na ajibu maswali yoyote ya kawaida.

b) RC au mtu wa kujitolea awaeleze watu walio na maswali maalum (kuhusiana na mahitaji au maswala yao wenyewe) kuyauliza katika Kituo cha Msaada (Help Desk) mara tu mkutano unakapomalizika.

c) Ujumbe huu lazima utangazwe kila wakati siku yote kila watu wapya waliohudhuria wanapofika; yanaweza kutangazwa wakati waliohudhuria wamepiga laini katika Kituo cha 1 na cha 2.



## **Hatua ya 5:** Msimamizi wa Benki ya Equity ashiriki ***Ujumbe Muhimu wa Benki*** na waliohudhuria mkutano wa jamii

Msimamizi wa Benki ya Equity atoa *Ujumbe muhimu wa Benki* kutoka kwa chapa iliyotolewa na Benki ya Equity. Hii ni pamoja na:

a) Maelezo ya hatua kwa hatua kuhusu kufungua kwa akaunti ya Benki na utoaji wa Kadi za ATM, ikiwa ni pamoja na mambo yatakayotendeka katika Vituo hivyo vitatu;

b) Wakati Kadi zitakuwa tayari kuzitumia;

c) Jinsi watu wasio na vitambulisho watawezesha Kadi zao za ATM kutumika mara tu wanapopata vitambulisho vya Kitaifa;

d) Jinsi ya kutumia Kadi za ATM;

e) Nini cha kufanya mtu anapopata matatizo na Kadi za ATM;

f) Si lazima kutoa pesa zote mara moja; ukiwa na akaunti ya Benki pesa zitabaki hapo kama hazijatumika kwa muda wa miezi 6.

g) Maajenti wa kulipa pesa za HSNP hawapaswi kulipisha ada yeyote ya kutoa pesa; lakini Benki italipisha ikiwa shughuli zitazidi 2 kwa miezi miwili.

Kisha Msimamizi wa Benki ya Equity aanzishe kazi ya ufunguzi wa akaunti ya Benki na awaongoze waliohudhuria kwenye vituo.





## III. Ujumbe wa Benki: Utatolewa na Msimamizi wa Timu ya Nyanjani wa Benki ya Equity

**Ikiwa umechaguliwa kuwa mwakilishi wa nyumba na ili ukamilishe ufunguzi wa akaunti ya benki, unatakiwa kutekeleza yafuatayo:**

- Kutoa kadi yako ya Kitambulisho cha Taifa au Risiti ya Usajili wa Nyumba ili zitolewe nakala (scanned);
- Kutoa habari ya kukamilisha kujaza fomu ya ufunguzi wa akaunti ya Benki;
- Kuchukuliwa nakala ya alama za vidole zako;
- Kupigwa picha yako ya dijitali ili ionyeshwe kwenye kadi ya ATM;
- Baada ya kazi ya ufunguzi wa akaunti ya benki kukamilika na ikiwa una kadi ya Kitambulisho halali , utapewa papo hapo kadi ya ATM na akaunti yako ya benki itawezeshwa kutumika katika muda wa siku kumi (10). Utaweza kupata fedha zako katika kipindi kinachofuata cha malipo kupitia agenti wa malipo wa Equity wa eneo lako au, kwenye Tawi lolote la Benki ya Equity au pia ATM ikiwa una PIN.
- Risiti za usajili wa Nyumba zitabaki na Ofisa wa Equity mara utakapokamilisha kufunguwa kwa akaunti.
- Kwa kundi la 1 (Group 1) la wasio na Vitambulisho, akaunti zenu zitawezeshwa mara tu mtakapopata vitambulisho. Wasilisha Kitambulisho chako kwa agenti wa eneo lako wa malipo ya Equity, ambaye atachukua picha (pande za mbele na nyuma) kwa kutumia simu ya mkononi (mobile phone) iliyo na kipengele maalum. Picha ya Kitambulisho chako itatumwa Benki ya Equity, Nairobi na akaunti yako itawezeshwa kutumika. Tutakapowezesha akaunti yako, utaanza kupokea malipo yako katika kipindi cha malipo kitakachofuata.
- Kwa Kikundi cha 2 (Group 2 scale up) cha watakaonufaika, pesa zitawekwa kwenye akaunti kulingana na maelekezo kutoka NDMA wakati wa upanuzi na mipango mingine ya dharura kwa mfanowakati wa ukame.



## Uandikishaji wa vitambulisho cha Taifa:

- Kama hauna vitambulisho halali cha Taifa, HSNP itakusaidia kukipata. Shughuli yauandikishaji wa vitambulisho cha Kitaifa utafanyika katika lokisheni yetu ndogo,wakati mmoja na ufunguzi wa akaunti ya benki.

- Tafadhali jitokezeni kwa wingi ili mhakikishe kuwa mmejiandikisha. Waambieni wengine ujumbe huu.

- Mahali, tarehe na muda wa shughuli hii, mtaelezwa na machifu na pia kupitia redio za jamii.

- Kamati ya uchunguzi itakaguwa wale wanaojiandikisha kulingana na sheria ya Kenya.

- Uchunguzi na uandikishaji wa vitambulisho utatolewa bila malipo. Tafadhali ripoti kwa chifu ikiwa utaona au kuskia mtu yeyote akilipisha au kutoa habari ya kupotosha.

- Baada ya kujiandikisha, utapokea Kitambulisho chako baada ya miezi miwili. Mara utakapopokea Kitambulisho chako, tafadhali nenda kwa agenti wa kutoa malipo wa Equity ambaye atakusaidia kuwezesha akaunti yako kwa kutuma picha ya kadi yako kwa simu ya mkononi (mobile) kwa Benki ya Equity, Nairobi.

## Ujumbe kuhusu haki yako

Masuala ambayo yanaweza kuathiri upataji wa pesa zako
Baadhi ya masuala ambayo yanaweza kuathiri kupata pesa zako na ambayo unahitaji kuripoti kwa RC ni pamoja na:

- Kadi kupotea au kadi iliyoharibika
- PIN kupotea
- Kifo cha mwakilishi wa nyumba
- Talaka katika nyumba
- Nyumba inayoongozwa na mtoto
- Malipo ya nyuma
- Ukosefu wa pesa katika akaunti ya benki ya wanaonufaika wakati wa kipindi cha malipo
- Ukosaji wa pesa za kutosha ya agenti wa Equity
- Agenti wa Equity kujishughulisha na matendo yasiyokubaliwa (kulipisha malipo ya pesa, kukataa kukupatia risiti baada ya kutoa pesa, kupokonya kadi yako na kadhalika)
- Ukosefu wa kupata agenti wa Equity



## **Hatua ya 6:** Ukusanyaji wa data na utoaji wa Kadi

Wakilishi wa Nyumba (recipients) watafuata laini katika Vituo 3:

**Kituo cha 1:** Afisa wa Benki ya Equity:

- athibitishe uhalali wa Kitambulisho cha Taifa au Risiti ya usajili wa Familia (Household Registration Reciept),
- achukue Fomu ya maombi ya akaunti ya Benki, na amsaidie Mwakilishi wa Nyumba kuikamilisha.

**Kituo cha 2:** Afisa wa Benki ya Equity akusanye maelezo yanayohitajika kutoka Mwakilishi wa Nyumba:

- Fomu ya Maombi ikiwemo sahihi
- Kitambulisho cha Taifa (pande zote) au Risiti ya Usajili wa Nyumba
- Biometriki (alama za vidole)
- Picha ya Dijitali

Afisa wa Benki ya Equity ampe Mwakilishi wa Nyumba risiti iliyokatwa kutoka Fomu ya maombi ya akaunti ya Benki.

**Kituo cha 3:** Afisa wa Benki ya Equity achapishe na kuweka data kwenye Kadi ya ATM Mwakilishi wa Nyumba arejeshe risiti ili apate Kadi ya ATM.

## **Hatua ya 7:** Msimamizi wa Benki ya Equity afunge eneo la kazi ya nyanjani

Msimamizi wa Benki ya Equity afunge eneo la kazi kulingana na maelekezo na mafunzo ambayo tayari amepokea kutoka Benki ya Equity.

## **Hatua ya 8:** Msimamizi wa Benki ya Equity na RC waripoti matatizo au masuala yoyote

Msimamizi wa Benki ya Equity na RC kila mmoja aripoti matatizo yoyote au masuala yaliyotokea katika kazi hilio fanywa kwa wasimamizi wao na Meneja wa Mradi wa HSNP (HSNP County Managers) katika Kaunti zao.

## Ujumbe muhimu wa Ufunguzi wa akaunti ya Benki

Kuna aina nne (4) za kutoa ujumbe muhimu wakati wa mkutano wa Jamii:

| Chifu au Msaidizi wa Chifu | RC au Mtu wa Kujitolea | Msimamizi wa Benki ya Equity |
|---|---|---|
| • Ujumbe muhimu wa mradi wa HSNP2 | • Ujumbe wa kindani wa mradi wa HSNP<br>• Ujumbe kuhusu haki | • Ujumbe kuhusu Benki |

## I. **Ujumbe muhimu wa mradi wa HSNP:** unatolewa na Chifu au Msaidizi wa Chifu

- Umealikwa hapa leo na mradi wa Hunger Safety Net Programme yaani HSNP, mpango wa Serikali unaosimamiwa na NDMA.
- Leo, HSNP inakufungulia akaunti ya Benki ya Equity Bank na kukupatia kadi ya ATM.
- HSNP imetekelezwa katika maeneo ya Turkana, Wajir, Marsabit na Mandera tangu mwaka wa 2008.
- HSNP kwa sasa iko katika awamu ya pili (2) na inatekelezwa na Serikali ya Kenya (GoK) kwa msaada wa Serikali ya Uingereza (UKAID) na Australia (DFAT).
- Timu ya ufunguzi wa akaunti zenu na utoaji kadi iko hapa na itakuwa hapa kwa muda wa siku XX.
- Tafadhali shirikianeni nao na mwajulishe wengine ambao bado hawajafungua akaunti za benki.
- Kutambulishwa kwa Timu.
- Ikiwa kutatokea suala lolote, tafadhali tembelea Kituo cha Msaada (Help Desk) au uje kwangu.





## II. **Ujumbe wa kindani wa mradi wa HSNP:** unatolewa na RC au mtu wa kujitolea

### Ufunguzi wa akaunti za Benki:

- HSNP ilitekeleza uandikishaji wa nyumba zote katika Kaunti yetu katika mwaka wa 2011

Orodha ya nyumba zilizochaguliwa kunufaika zilijulishwa kwenu na mfanyakazi wa NDMA.

- HSNP hutoa msaada wa kifedha kila baada ya miezi (2), kupitia akaunti ya benki kwa nyumba za wale waliotambuliwa na HSNP kama maskini sana na wanaoishi katika mazingira magumu.
- HSNP inaweza pia kutoa pesa za muda kwa baadhi ya nyumba zaidi zinazoishi katika mazingira magumu ikiwa kuna jambo la dharura, kama ukame.
- Ili ufungue akaunti, lazima uwe na Kitambulisho halali cha Taifa. Kama huna kitambulisho, bado unaweza kufungua akaunti.
- Utapatiwa Risiti ya usajili wa Nyumba (Household Registration Reciept) kutoka kwa RC au Mtu wa Kujitolea katika Kituo cha Msaada (Help Desk), yaani ikiwa bado hujapokea.
- Huduma ya kufungua akaunti ya benki na Risiti za usajili hutolewa bila malipo. Hupaswi kulipa ili uwe kwenye mradi wa HSNP.







HSNP2: Mwongozo wa Nyanjani 2014

HUNGER SAFETY NET PROGRAMME | NDMA 17TH FLOOR, LONHRO HOUSE, NAIROBI | www.hsnp.or.ke

# HSNP2:
# Mwongozo wa Nyanjani

**Kufungua akaunti ya benki, kupokea kadi za ATM, Uandikishaji wa vitambulisho vya taifa na Kusuluhisha matukio maaluum**

Mradi wa HSNP unatekelezwa katika Kaunti za Turkana, Mandera, Wajir na Marsabit. Kikundi cha kwanza cha 100,000 kitapata msaada wa fedha kila ya miezi miwili. HSNP pia inaweza kutoa fedha za muda kwa baadhi ya nyumba zaidi zinashoishi katika mazingira magumu ikiwa kuna jambo la dharura, kama ukame. HSNP ni mradi wa Serikali ya Kenya,unaosimamiwa wa NDMA na kufadhiliwa na serikali za Kenya, Uingereza na Australia.

.

HUNGER SAFETY NET PROGRAMME | NDMA, 17TH FLOOR, LONHRO HOUSE, NAIROBI | www.hsnp.or.ke